
# WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI




## Kitabu Cha Katuni kuhusu Umuhimu na Manufaa ya Anwani za Makazi na Postikodi Nchini

*Tumia Anwani za Makazi kwa Maendeleo ya Kiuchumi na Kijamii*

# BODI YA WAHARIRI



**Mwenyekiti**

**Dkt. Zainabu A. S. Chaula**
Katibu Mkuu Wizara ya Habari,
Mawasiliano na Teknolojia ya Habari



**Mratibu na Mhariri wa Kitabu**

**Prisca J. Ulomi**
Mkuu wa Kitengo cha
Mawasiliano Serikalini

**Wasanifu Kitabu**

**Prisca J. Ulomi**
**Faraja Mpina**
**Chedaiwe Msuya**
**Janeth Peter**

**Mchora Katuni**

**Masoud Kipanya**

## DIRA NA DHIMA

### DIRA

Kuwa na jamii iliyowezeshwa Kidijitali kwa Maendeleo ya Kiuchumi na Kijamii.

### DHIMA

Kuwezesha utoaji wa huduma za uhakika na gharama nafuu za Teknolojia ya Habari, Mawasiliano ya simu na Posta kwa kuweka mazingira yanayokuza ubunifu katika kuibadilisha Tanzania kuwa na Uchumi wa Kidijitali.

# TAHARIRI

## DHANA NZIMA YA MFUMO WA ANWANI ZA MAKAZI NA POSTIKODI

Anwani za Makazi ni mfumo unaotambulisha mahali halisi ambapo mtu anaishi, mahali ilipo biashara yake au ofisi anayofanyia kazi kwa kufuata jina la barabara na mtaa, namba ya nyumba au jengo pamoja na Postikodi. Postikodi au simbo za posta kama inavyotambulika ni mfumo maalum wa tarakimu unaotambulisha eneo la kufikisha huduma za posta ambapo kwa nchi ya Tanzania inaanzia katika ngazi ya kata, wilaya, mkoa na kanda.

Serikali kupitia Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi inatekeleza mradi wa Anwani za Makazi na Postikodi nchini lengo likiwa ni kurahisisha mawasiliano, ufikishaji wa huduma za Serikali kwa wananchi na kufanyika kwa shughuli za kijamii, kiuchumi na kiutawala.

Wengi wetu tukisikia neno 'Anwani' mawazo yetu yanakwenda moja kwa moja kwenye sanduku la barua la posta kama anwani kitu ambacho ni sahihi, lakini tunapozungumzia Mfumo wa Anwani za Makazi na Postikodi tunaongelea miundombinu ambayo inawekwa na Serikali ili kurahisisha kumfikia mtu mahali alipo iwe nyumbani kwake, ofisini kwake au eneo analofanyia biashara kwa kufuata anwani ya makazi ya mhusika inayojumuisha jina ya barabara, mtaa, namba ya nyumba au jengo na postikodi.

Kutokana na maendeleo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) matumizi ya sanduku la barua la posta kama anwani yamepungua nchini, lakini kwa upande mwingine matumizi ya Mfumo wa Anwani za Makazi na Postikodi yamefungamana na TEHAMA na itawezesha huduma za posta kuendelea kuleta tija na kukuza uchumi wa mwananchi moja moja na nchi kwa ujumla.

Mfumo wa Anwani za Makazi pia unapatikana kupitia programu tumizi ya simu za mkononi inayoitwa NAPA Mobile App ambayo inaingizwa taarifa zote za makazi ya watu, majengo ya ofisi za Serikali na Binafsi, barabara, njia, majina ya vituo vinavyotoa huduma za kijamii kama hospitali, shule, zahanati n.k na inafanya kazi kama google map, ambapo mwananchi anaweza kuingia kwenye programu hiyo kupitiasimu ya mkononi na kuandika mahali anapotaka kwenda kutoka mahali alipo kwa muda huo na programu hiyo itamuonesha njia ya kupita mpaka kufika sehemu husika.

Aidha matumizi ya mfumo wa Anwani za Makazi na Postikodi unarahisisha ufanyikaji wa biashara mtandao kwa kuuza au kununua bidhaa kwa njia ya mtandao na kuletewa mpaka mlangoni; kurahisisha ufanyikaji wa huduma za posta na usafirishaji wa bidhaa na abiria mfano uber, bolt; unarahisisha ufikishaji wa huduma za Serikali kwa wananchi kama vile huduma za zimamoto, polisi, gari ya kubebea wagonjwa, sensa ya watu na makazi; kurahisisha makusanyo ya kodi za Serikali; na shughuli zote za kiutawala, kijamii na kiuchumi.


Dhana nzima ya uwekaji wa Mfumo wa Anwani za Makazi na Postikodi nchini licha ya kuwa ni utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Posta ya mwaka 2003 inayotaka nchi kuwa na Anwani za Kitaifa zitakazowezesha ufikishaji wa huduma mbalimbali kwa wananchi, pia ni maelekezo ya Kimataifa ya Umoja wa Posta Afrika (PAPU) na Umoja wa Posta Duniani (UPU) pamoja na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya 2020 – 2025.

Ni jukumu la kila mwananchi kulinda, kuitunza na kuitumia vema miundombinu ya Anwani za Makazi na Postikodi kwa kutambua na kuthamini umuhimu wake wa kuwezesha uendeshaji wa shughuli mbalimbali za kijamii, kiuchumi na Serikali kwa maendeleo ya Taifa letu.

# Unapoishi panaelezeka..?




HALOO! WE MBONA MZITO KUELEWA!? NIMEKWAMBIA UKIUPITA MPAPAI MBELE KUNA MAMA ANAUZA MIHOGO KATA KUSHOTO!
MPAPAI UKIKATWA, KWAKO KUNAELEKEZEKA?
UNAPOISHI PANAELEKEZEKA?


ALIYEAGIZA HUU MZIGO MTANDAONI ALISEMA NIKIFIKA MTAA WENYE MITI MINGI NITAONA NYUMBA KUNA UGOMVI, NDO HAPO!
NI KWELI HAPA KULIKUWA NA UGOMVI LAKINI HATUJAAGIZA MZIGO WOWOTE
UNAPOISHI PANAELEKEZEKA?


UMESEMA NIKIFIKA MTAA WENYE MATEJA WENGI NIINGIE KUSHOTO?
TWENDE DEREVA, NDO HAPA..
UNAPOISHI
PANAELEKEZEKA?


MATANGAZO NALIPIA LAKINI WATEJA SIWAONI
TEMBELEA DUKA LETU LIPO MIVINJENI KARIBU NA DAMPO, NYUMA TU YA GETI LA POLISI, ULIZIA KWA KIBONGE, UKIFIKA KWAKE MUULIZIE MTU YOYOTE ATAKULETA..
UNAPOISHI PANAELEKEZEKA?



NENDA STREIT, MTAA WA KWANZA UACHE, WA PILI UACHE, WA TATU UACHE, INGIA WA NNE UMEFIKA KWA KIPANYA!
DOH!
UNAPOISHI
PANAELEKEZEKA?


MTU ALIYEPIGA SIMU ALISEMA NI MTAA WENYE FREMU NYINGI! HAPA KILA MTAA UNA FREMU NYINGI!
FIRE
UNAPOISHI PANAELEKEZEKA?


WANANCHI TUTARUHUSIWA KUTOA MAJINA YA MITAA YETU?
KUNA UTARATIBU UTATOLEWA
KIPANYA STREET


NI LAZIMA MAJINA YA MITAA AU BARABARA YAWE NI YENYE HERUFI?
NAMBA PIA ZINAWEZA KUTUMIKA, KWA MFANO, BARABARA YA SITA..



MAJINA YASIYOFAA KIMAADILI YANAPASWA KUEPUKWA!
MSAGAJI STREET


UTARATIBU WA ANUANI ZA MAKAZI HAUTOFIKA KWA WAKAAZI WA MABONDENI..
DAH!!


9
8
MZIGO WANGU ULETWE KIGAMBONI, CLOUDS CITY, MTAA WA POWERBREAKFAST NYUMBA NAMBA TISA.


WANANCHI WANA UWEZO WA KUKATAA JINA LA MTAA?



KWA MFANO MTAANI KWETU WAKAAZI WENGI WACHAGA! HATUWEZI KUUITA MTAA WETU WACHAGA FOREVA?
AU WACHAGA ONLI STRIIT
MAJINA YANAYOWEZA KUENDELEZA UDINI, UKABILA AU KUFANYA MAENEO KUWA YA KISIASA YANAPASWA KUEPUKWA


KAMA BARABARA INAINGIA KWENYE NYUMBA YAKO TU HAIWEZI KUPEWA JINA LA MTAA
KAMA MTAA HUO UNA NYUMBA ZAIDI YA MOJA UNAWEZA KABISA KUPEWA JINA LA MTAA.
OK..


UTARATIBU WA KUTOA MAJINA YA MITAA UKOJE?
UNAANZIA NGAZI YA MTAA/KITONGOJI, KIJIJI, KAMATI YA MAENDELEO YA KATA...
Kamati ya Kudumu ya masuala ya mipango miji na mazingira na hatimaye Baraza la Madiwani. Halmashauri itawajibika kutoa taarifa kwa wadau wote juu ya majina ya mitaa yaliyoidhinishwa na kuingizwa katika Daftari la Kudumu la Majina ya Barabara/mitaa katika Halmashauri husika.


WANANCHI AMBAO TAYARI MTAA WAO UNA JINA WANAO UWEZO WA KUBADILISHA JINA?


BABA, LEO NIMESIKIA KUHUSU POSTIKODI, NI NINI HIYO?


KWANI KUNA AINA NGAPI ZA ANUANI?
KUNA AINA TATU KUU ZA ANUANI ZINAZOTUMIKA DUNIANI KOTE..
1. ANUANI ZA KIJIOGRAFIA ambazo hutumia mifumo ya urejeleaji (kwa mfano longitudo na latitudo) kutoa maelezo sahihi na ya kudumu ya mahali kitu kilipo duniani.
2. ANUANI YA POSTA hutumia taarifa za mahali halisi ili kufikisha bidhaa za kiposta au kifurushi (mfano: Sanduku la Posta).
3. ANUANI YA MAKAZI hutumia majina ya barabara/ mitaa na namba za nyumba kuonesha mahali sahihi, kamili, pa kudumu na mahususi kitu kilipo.


VIJIJINI PIA KUNA MITAA, MPANGO WA ANUANI ZA MAKAZI UTAFIKA VIJIJINI?


KWA MFANO, KIKUNDI CHA WAJERUMANI WANAOISHI ENEO MOJA WANATAKA KUTUMIA MFUMO WAO INARUHUSIWA?
ILI KUONDOA MKANGANYIKO, MFUMO UTAKAO TUMIKA NI MMOJA TU.




Kama jina la mtaa lililopendekezwa litakataliwa na Halmashauri kwa sababu yoyote ile, suala hilo linapaswa kujadiliwa na kukubaliwa na pande zote zinazohusika. Kama hakutakuwa na maafikiano baina ya pande hizo, upande usioridhika unaweza kukata rufaa kwa maandishi kwa Katibu Tawala wa Wilaya, ikishindikana katika ngazi hii ikatwe rufaa kwa Katibu Tawala wa Mkoa ambaye uamuzi wake utakuwa wa mwisho.


NATAKA MTAA WETU TUUPE JINA LAKO..
LINAWEZA KUFIKIRIWA ENDAPO LINA HISTORIA NA ENEO, AU KAMA ALITOA BURE ENEO..
KIPANYA STREET


MAJINA YANAYOASHIRIA CHUKI, UVUNJIFU WA AMANI, HAYATORUHUSIWA
SIWAPENDI WAZARAMO STREET


MOJA STREET
INAPOBIDI, KANUNI ZINAIPA MAMLAKA YA UPANGAJI NGUVU YA KUWEKA JINA LA MTAA KWENYE SEHEMU YA UKUTA WA NYUMBA YAKO


A
B
C
D



Limeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari
S.L.P. 677,40470 Dodoma, Tanzania
Barua pepe: ps@mawasiliano.go.tz
Tovuti: www.mawasiliano.go.tz
Instagram: Wizarahmth
Twitter: Wizarahmth